**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

**CHUO CHA MAENDELEO YA JAMII UYOLE**

Kumb. No: CDTI/UY/T.20/VOL.VIII/021 1 Julai, 2026

Ndugu,…………………………………………………………………….

…………………………………………………………………….

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA CHETI/ ASTASHAHADA YA MAENDELEO YA JAMII (NTA 4) KWA MWAKA WA MASOMO 2026/2027**

**1.0** Ninayo furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga katika mafunzo ya taaluma ya Maendeleo ya Jamii (NTA 4) ngazi ya Cheti/Astashahada katika **Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole**. Mafunzo haya ni ya muda wa miaka mitatu (3), na yatakuwezesha kupata stashahada katika fani tajwa hapo juu baada ya kushiriki kikamilifu katika mafunzo ya nadharia darasani na vitendo (Field Practical Training) kwa muda uliopangwa.

**2.0** Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole kinapatikana Uyole, Jiji la Mbeya, Mkoa wa Mbeya, kando ya barabara kuu ya Mbeya–Tukuyu.

**3.0** Chuo kitafunguliwa tarehe **13/10/2026**. Unatakiwa kuripoti chuoni kuanzia tarehe hiyo na si baada ya tarehe **30/11/2026**. Iwapo hautakuwa umeripoti chuoni kufikia tarehe hiyo bila sababu za msingi, nafasi yako ya masomo inaweza kutolewa kwa mwombaji mwingine.

**4.0** Unatakiwa kuwasilisha stakabadhi za malipo ya ada na gharama nyingine zinazohusiana na mafunzo yako mara utakapofika chuoni. Malipo yote yatafanyika kwa kutumia Nambari ya Kumbukumbu ya Malipo **(Control Number)** ambayo utapatiwa baada ya kuwasiliana na Ofisi ya Utawala na Fedha. Aidha, malipo mengine yatakayohitajika kufanywa kupitia akaunti za chuo yataelekezwa rasmi mara utakapowasili chuoni.

**5.0** Gharama zote za usafiri wa kwenda chuoni na kurudi nyumbani katika mihula yote ya masomo zitagharamiwa na mwanafunzi au mlezi/mzazi wake.

**6.0** Mwanafunzi anatakiwa kufika chuoni akiwa na nyaraka na mahitaji yafuatayo:

- Vyeti halisi vya elimu ya sekondari au taarifa rasmi ya matokeo ya mtihani (Results slip).
- Picha tatu (3) za pasipoti (Passport size) za hivi karibuni.
- Cheti cha kuzaliwa.
- Rimu moja (1) ya karatasi za A4.

- Blanketi, shuka, mto wa kulalia, ndoo na nguo za michezo.
- Kwa kuwa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole kipo katika eneo lenye hali ya hewa ya baridi, wanafunzi wanashauriwa kuja na mavazi ya kujikinga na baridi.

**7.0 Usafi wa mazingira:** Kila mwanafunzi anatakiwa kushiriki katika shughuli za usafi wa mazingira na utunzaji wa miundombinu. Aidha, atawajibika kuhakikisha usafi wa maeneo ya kuishi, vyumba vya kulala na mazingira mengine ya chuo ili kudumisha mazingira yanayofaa kwa kujifunzia na kuishi.

**8.0 Malazi:** Chuo kina mabweni hivyo, wanafunzi watakaohitaji huduma ya malazi watapangiwa nafasi kulingana na utaratibu wa chuo. Gharama zimeainishwa katika fomu hii.

**9.0 Utambulisho wa Awali (Orientation):** Mara utakapowasili chuoni, utapatiwa kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali ya chuo. Aidha, utashiriki programu ya utambulisho wa awali (Orientation) itakayokuwezesha kufahamu mazingira ya chuo.

**10.0 Utaratibu wa Mavazi:** Wanafunzi wote wanatakiwa kuvaa sare rasmi wakati wa vipindi vya darasani. Aidha, wanatakiwa kuvaa T-shati ya chuo katika siku zitakazopangwa na uongozi wa chuo. T-shati zinapatikana chuoni kwa gharama ya shilingi **25,000/=,** na gharama zake zimejumuishwa katika michango mingine iliyoainishwa katika waraka huu.

- ✓ **Sare kwa wanaume** – Suti mbili (2): Suruali na koti rangi ya dark blue (pair 1), Suruali na koti rangi nyeusi (pair 1) na mashati light blue (moja) na nyeupe (moja), na viatu vya kufunika.

**11.0 Sare kwa wanawake** – Suti mbili (2): Sketi na koti rangi ya dark blue (pair 1), Sketi na koti rangi nyeusi (pair 1) na mashati light blue (moja) na nyeupe (moja), na viatu vya kufunika. Sketi itashonwa mshono wa **SMART** yenye mpasuo wa kufunika nyuma.

## 12.0 Kukubali Nafasi ya Masomo

Iwapo unakubaliana na masharti yaliyobainishwa katika waraka huu, tafadhali jaza na kusaini fomu ya kukubali nafasi ya masomo iliyoambatanishwa, kisha uiwasilishe kwa Ofisi ya Msajili wa Wanafunzi mara tu utakapowasili chuoni.

**12.0 Hitimisho na Mawasiliano**

Kwa mara nyingine tena, tunakupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na mafunzo ya Astashahada ya Maendeleo ya Jamii katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole.

Iwapo utahitaji maelezo au ufafanuzi Zaidi, tafadhali wasiliana na:

**Simu: 0714 862 998 (Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma)**

Tunakukaribisha Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole na tunakutakia mafanikio mema katika safari yako ya kitaaluma na maendeleo ya taaluma ya Maendeleo ya Jamii.

PRINCIPAL
COMMUNITY DEVELOPMENT TRAINING INST
UYOLE-MBEYA

……………………………………………

**MKUU WA CHUO**

**CHUO CHA MAENDELEO YA JAMII UYOLE**

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA YA MAENDELEO YA JAMII MWAKA WA MASOMO 2026/2027**

Mimi .......................................................................................................................

(Jina Kamili kwa Herufi Kubwa)

Tarehe ya Kuzaliwa: ........../........../............

Nathibitisha kuwa nimepokea taarifa ya kuchaguliwa kujiunga na mafunzo ya Astashahada ya Maendeleo ya Jamii katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole kwa mwaka wa masomo 2026/2027.

Ninaelewa na kukubali masharti yote ya kujiunga na mafunzo haya, na ninaahidi kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zote za chuo katika kipindi chote cha masomo yangu.

Sahihi ya Mwanafunzi: ..................................................

Tarehe: ........../........../............

**TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI/MDHAMINI**

Jina Kamili: ..........................................................................................

Anuani ya Makazi:

…………………………………………… Simu na: ........................................

.........................................

Sahihi: ........................................Tarehe: ........../........../................

The Medical Officer

…………………………………..

………………………………….

**PART: A**

Mr.Miss/Mrs ……………………………………………Please examine the above named students as to his/her physical and mental fitness for a full time student in this Institute. The Examination should include the following categories:-

1. Hemoglobin level………………………………..
2. P.V. bleeding………………………………..
3. Sight………………………......
4. Blood presser……………………………….
5. Urine for sugar ………………………………
6. Urine for pregnancy test ……………………………..
7. U.T.I……………………………….
8. Stool for routine Examination………………………………
9. Asthma ..……………………………..
10. Skin disease………………………………
11. Any Deformity……………………………….
12. Pulmonary tuberculosis (PTB)………………………………
13. Leprosy………………………………
14. Epilepsy………………………………
15. Neurosis………………………………
16. Sexually transmitted infections (STI'S)………………………………
17. Other permanent disease………………………………

**PART: B**

**MEDICAL CERTIFICATE:**

(To be completed by a Government Medical Officer)

1. I have examined the named student and consider that he/he is physically, mentally fit or unfit.
2. Other comments.
   ……………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………

Date …………………………  Signature…………………..

Designation …………………  Station………………………

**UTARATIBU WA MALIPO YA ADA NA MICHANGO MINGINE KWA WANAFUNZI WA MWAKA WA I (NTA 4)**

## 1. MCHANGANUO WA MALIPO YA ADA

| AWAMU ZA MALIPO | KIASI | TAREHE YA MALIPO |
|---|---|---|
| AWAMU 1 | 150,000 | 13 Oktoba - 31 Oktoba, 2026 |
| AWAMU YA 2 | 150,000 | 1 Novemba - 30 Disemba, 2026 |
| AWAMU YA 3 | 150,000 | 1 Mei – 31 Juni, 2027 |
| AWAMU YA 4 | 150,000 | 1 Julai – 31 Julai, 2027 |
| **JUMLA YA ADA KWA MWAKA** | **600,000** | |

## 2. MCHANGANUO WA MALIPO YA MICHANGO MINGINE

| AWAMU YA MALIPO | AINA YA MALIPO | KIASI | TAREHE YA MALIPO |
|---|---|---|---|
| **AWAMU YA KWANZA** | Usajili | 15,000 | 13 Oktoba - 31 Oktoba 2026 |
| | Kitambulisho | 10,000 | |
| | NACTVET Quality Assurance fee | 20,000 | |
| | Student organisation | 10,000 | |
| | T-shirt | 25,000 | |
| | NHIF | 50,4000 | |
| | **JUMLA YA AWAMU YA 1** | **130,400** | |
| **AWAMU YA PILI** | Examination Fee | 30,000 | 1 Novemba - 30 Disemba 2026 |
| | **JUMLA YA AWAMU YA PILI** | **30,000** | |
| **AWAMU YA TATU** | Uchakavu | 10,000 | 1 Mei – 31 Juni, 2027 |
| | Huduma ya Kwanza | 10,000 | |
| | Certificate and Transcript | 15,000 | |
| | **JUMLA YA AWAMU YA TATU** | **35,000** | |
| **JUMLA YA MICHANGO MINGINE KWA MWAKA** | | **195,400** | |

**<u>KUMBUKA:</u>**
**JUMLA KUU YA ADA NA MICHANGO MINGINE KWA MWAKA NI 795,400**

## 3. MCHANGANUO WA MICHANGO KWA WANAFUNZI WA BWENI

| MALIPO/MUHULA | AWAMU YA KWANZA | AWAMU YA PILI | MUHULA WA PILI | JUMLA YA MWAKA |
|---|---|---|---|---|
| Ada ya Bweni | 100,000 | 100,000 | | 200,000 |
| Fedha ya Chakula | 425,000 | | 425,000 | 850,000 |
| **TAREHE YA MALIPO** | **13 Oktoba-31 Oktoba 2026** | **1 Novemba - 30 Disemba 2026** | **1 Mei – 31 Juni, 2027** | **1,050,000** |

## 4. GHARAMA NYINGINE

**Zingatia:** Gharama hizi zitatolewa na mzazi/mlezi kwa mwanafunzi mwenyewe, kwa ajili ya kumuwezesha kugharamia huduma mbalimbali zitakazohitajika wakati wa masomo, hivyo hazitalipwa chuoni)

| GHARAMA | KIASI | MAELEZO |
|---|---|---|
| Mazoezi kwa vitendo (Field) | 300,000 | Mzazi/mlezi atampatia mwanafunzi wakati wa Field |
| Gharama za viandikwa (Stationery) | 150,000 | Mzazi/mlezi atampatia mwanafunzi kwaajili ya matumizi ya Stationery kwa mwaka wa masomo |

## 5. MAMBO YA KUZINGATIA

1. HAKIKISHA UNAFUATA MAELEKEZO YOTE YA MALIPO KAMA YALIVYOELEKEZWA ILI KUEPUKA USUMBUFU WAKATI WA USAJILI NA KURIPOTI CHUONI
2. ADA NA MICHANGO MINGINE INAWEZA KULIPWA KWA MKUPUO AU KWA AWAMU, KULINGANA NA RATIBA YA MALIPO ILIYOAINISHWA KATIKA WARAKA
3. MWANAFUNZI ATAPORIPOTI ATATAKIWA KUKAMILISHA MALIPO YA AWAMU YA KWANZA ILI ASAJILIWE KAMA YALIVYO ORODHESHWA KATIKA JEDWALI NAMBA 1 NA NAMBA
4. KWA MWANAFUNZI ATAKAE KAA BWENI ATATAKIWA KUTHIBITISHA KWANZA KABLA YA KUFANYA MALIPO (Nafasi ni chache)